

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HW/.....

Tarehe:

BAHI ENGLISH MEDIUM PRE & PRIMARY SCHOOL

S. L. P 2993,

BAHI - DODOMA.

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

.....
S.L.P.....
.....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA MSINGI BAHI
ENGLISH MEDIUM ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI
MKOANI DODOMA KWA DARASA LA AWALI, DARASA LA KWANZA NA
DARASA LA PILI MWAKA 2023**

1.0 UTANGULIZI

Shule ya msingi Bahi English Medium ni shule ya kutwa ya serikali ya mchepuo wa Kiingereza (English Medium) inayomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ipo katika kata ya Bahi kilometra 1(moja) kutoka Bahi mjini.

2.0 MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

2.1 SARE YA SHULE (SCHOOL UNIFORM)

**VINAVYOPATIKANA SHULENI NI KAMA VIFUATAVYO KWA
GHARAMA TAJWA:-**

- ❖ Kaptula mbili za draft yenyewe mchanganyiko wa bluu bahari na damu ya mzee. (kwa wavulana) Tsh.20,000/=@moja.
- ❖ Sketi mbili zilizoshonwa kwa mwonekano wa rinda boksi yenyewe saspenda za drafti zenyewe mchanganyiko wā rangi ya bluu bahari na damu yamzee (kwa wasichana)Tsh.20,000=@moja .
- ❖ Mashati mawili rangi ya bluu Bahari mikono mifupi yenyewe nembo ya shule Tsh.13,000/=@moja.
- ❖ Sweta moja (rangi ya damu ya mzee) Yenyewe nembo ya shule Tsh.15,000/=@moja.
- ❖ Track suit (rangi ya dark bluu yenyewe mchirizi mweupe ubavuni) itavalawa siku ya Jumatano na ijamua pamoja na fulana (T-shirt) Tsh.20,000/=
- ❖ T-shirt nyeupe yenyewe kola dark blue yenyewe nembo ya shule (Fulana) Tsh.10,000/=
- ❖ Tai Tsh.2,000/=

NB; MZAZI ATAVINUNUA NJE YA SHULE

- ❖ Raba za michezo (rangi nyeupe) zitavalawa siku ya ijamua.
- ❖ Soksi nyeupe jozi mbili
- ❖ Viatu vyeusi jozi mbili

NB: Gharama za vifaa vinavyopatikana shule vitalipiwa shulenii kwa fedha taslimu.

2.2 MAHITAJI MENGINE

- ❖ Vifaa vya kujifunzia (Daftari, Kalamu, nk)
- ❖ Rimu moja ya karatasi kwa mwaka (A4) iwasilishwe Shulenii

3.0 MICHANGO YA SHULE

- i. Michango ya chakula kwa mwaka ni shilingi laki mbili na hamsini elfu (**250,000/=**)
- ii. Ada ni shilingi laki mbili na hamsini elfu (**250,000/=**) kwa mwaka kwa wanafunzi wote
NB: Michango yote italipwa kwa awamu mbili yaani (Januari na Julai) shule inapofunguliwa. Mzazi atakaye shindwa kumlipia mtoto wake michango ya shule kwa wakati mtoto atahamishiwa shule za Mfumo wa Kiswahili.
Aidha michango yote ilipwe kupitia benki ya NMB kwa akaunti zifuatazo **52710013556**
BAHI ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL. Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi katika “Pay in Slip”

4.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- i. Wizi
- ii. Kugombana mwanafunzi kwa mwanafunzi
- iii. Kudharau alama za Taifa kama bendera ya Taifa, fedha, picha ya Rais, nk
- iv. Uhariibifu wa mali ya umma kwa makusudi
- v. Kugomea adhabu halali ya mwalimu au kiranya

5.0 SHERIA, TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE

Kila mwanafunzi itampasa kufuata taratibu na kanuni za shule hii kama zilivyoonyeshwa hapo chini.

5.1. TARATIBU ZA MASOMO

Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shule inapofunguliwa na kuzingatia mambo yafuatayo:-

- i. Kuingia darasani mapema kulingana na ratiba kuu ya masomo
- ii. Kusimama na kusalimu mwalimu anapoingia darasani
- iii. Kuhudhuria vipindi vyote viliyopangwa katika ratiba kuu ya masomo
- iv. Kufanya majaribio, mazoezi na mahitaji yote yanayomuhusu
- v. Mwanafunzi atawajibika kujifunza na kuongea Kiingereza muda wote awapo shulenii ikiwa ni pamoja na kutekeleza kanuni ya **“SPEAK ENGLISH ONLY”**
- vi. Mwanafunzi anyooshe mkono wake juu na asimame wakati wa kuuliza au kujibu maswali.
- vii. Mwanafunzi atatakiwa kufanya majaribio na mitihani yote ya ndani na nje.

5.2 Ikiwa mwalimu hayupo darasani itampasa mwanafunnzi

- i. Kusoma kimya kimya darasani
- ii. Kutotembea ovyo
- iii. Kutotoka nje ya darasa bila sababu

5.3 MAADILI MEMA

5.3.1 Kila mwanafunzi wa shule hii atatakiwa

- i. Kuwahi kufika shulenii, kuheshimu Walimu, Wafanyakazi, Viranja wa shule na Wageni
- ii. Kusimama na kusalimu wakubwa/walimu wanapopita ama kuongea nao kwa lugha ya kiingereza

5.3.2 Wanafunzi wasitembee sehemu zifuatazo bila kibali

- i. Ofisi ya Walimu
- ii. Nyumba za Walimu

- 5.3.3 Mwanafunzi anatakiwa kuwa safi wakati wote kwa:-**
- i. Kuvaas sare za shule kwa kuchomekea shati ndani Suruali/Sketi
 - ii. Kukata nywele vizuri na kuzichana kwa wavulana na wasichana aidha wasichana wanaruhusiwa kusuka nywele vizuri (Twende kilioni au mnyosho)
 - iii. Kukata kucha na kuoga kila siku
 - iv. Kutovaa mapambo kama vile mikufu, heleni, bangili, shanga, kofia, kupaka rangi kucha, wanja, rangi za midomo, kuvaas pete n.k.

KARIBU SANA

